# TARGETER WINGS
# KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## GREDI YA 6 - MWAKA WA 2025
## SEHEMU A:
## KISWAHILI LUGHA

**Wings 001**

**Muda: Saa 1**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha Kiswahili na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30.
2. Ukisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

**NAMBA YAKO YA TATHMINI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**
**JINA LA SOMO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali **1 - 30** umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu sahihi.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali chagua jibu sahihi:**

**29.** ***Kamilisha methali:***
Lapendeza rangi lakini halikai.

A. Muwa        B. Mchele
C. Ua        D. Mayai

Jibu sahihi ni C.

**Katika karatasi ya majibu:**

**29.** [A] [B] [~~C~~] [D]    **30.** [A] [B] [C] [D]    **31.** [A] [B] [C] [D]    **32.** [A] [B] [C] [D]

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa

**Swali la 1 hadi la 5.**

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.**

***(Ni wakati wa alasiri. Timu ya soka ya shule ya pepeta inarejea kutoka mashindano. Kaka ndiye nahodha wa timu)***

**Kaka** : *(Akiimba kwa furaha)* Pepeta aaah, pepeta aah

**Mwalimu Mkuu** : *(Akisimama nje ya afisi yake)* Kuna nini?

**Kaka** : Sisi ndio washindi. Tumechapa timu ya Bembea mabao mawili kwa nunge.

**Mwalim Mkuu** : *(Kwa furaha)* Hongera <u>nahodha</u> kwa kweli umefanya bidii.

**Kaka** : Nashukuru mwalimu ila ushindi huu ni wetu sote. Tulitii kocha wetu na kufuata ushauri wake. Aidha achanikaye kwenye mpini hafi njaa. Tulijifunga kibwebwe na hatimaye tumeibuka na ushindi.

**Mwalimu Mkuu**: *(Akiwapongeza)* Kila mmoja wenu nitampa zawadi kesho kutwa.

**Kaka** : Asante mwalimu. Nakuomba kwa hisani yako utununulie vifaa zaidi vya spoti. Vitatuwezesha kukabiliana na wapinzani wetu vilivyo.

**Mwalimu Mkuu**: Hakika nyinyi ni majogoo. Naona kuwa kusudi lenu ni kutawazwa mabingwa wa kaunti hii.

**Kaka** : Ndivyo mwalimu. Tutaimiminia shule hii sifa kwa kuwa mabalozi wema.

**1.** Mwalimu Mkuu na Kaka walikutana alasiri. Je, kaka angemwamkua vipi mwalimu mkuu?

A. Shikamoo? B. Hujambo

C. Habari za jioni D. Masalkheri

**2.** Unafikiri ni kwa nini kakaa alikuwa akiimba?

A. Hakupenda masomo

B. Timu yake iliibuka na ushindi

C. Anashiriki katika kwaya ya shule

D. Alitaka mwalimu mkuu ajue wameshinda

**3.** Timu ya Pepeta ilishinda mechi yao kwa sababu ya

A. bidii ya kaka

B. bidii na utiifu wa wachezaji

C. juhudi za wachezaji na mwalimu mkuu

D. kufanya mazoezi mengi

**4.** Je, ikiwa shindano hili lilifanyika Jumanne, mwalimu mkuu angewapa zawadi wachezaji wa shule hii siku gani?

A. Jumatano B. Ijumaa

C. Jumanne D. Alhamisi

**5.** Neno, '**Nahodha**' limetumika katika mazungumzo haya. Neno jingine lenye maana sawa na Nahodha ni

A. kocha B. kiranja

C. kapteni D. mchezaji

**Swali la 6 hadi la 9**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Niliwasili nyumbani kwa nyanya jua likiaga miti. Nilikuwa na hamu kuu ya kusimuliwa hadithi. Hakika, nilipenda simulizi za nyanya kwa dhati ya moyo wangu. Giza lilipoanza kuingia nyanya alituandalia chajio. Tukala na binamu zangu. Nyanya alianza hivi: "Zamani za kale, Kima na Mamba walikuwa marafiki. Kima aliishi juu ya mwembe karibu na mto Naisula. Kama yalivyokuwa mazoea, Mamba alikwenda kumjulia hali rafiki yake. Kima alimkaribisha mgeni wake kwa embe tamu lililokuwa limeiva.

Mamba alikula embe hilo na hata kuramba vidole vyake. Alimshukuru Kima na kuanza kurudi nyumbani kwake. Njiani alijiambia, "lazima moyo wa Kima uwe ni mtamu sawa na embe alilonipa kwa kuwa yeye hula maembe kila siku." Aliamua kumpangia rafiki yake njama.

Alirudi kwa Kima siku iliyofuata na kumshukuru tena kwa ukarimu wake. Alimshawishi Kima ambaye hakujua kuogelea amtembelee nyumbani kwake. Alimbeba mgongoni. Walipofika katikati ya mto, Mamba akamwambia Kima, "leo lazima niule moyo wako." Kima alishikwa na woga akashindwa na la kufanya. Kwa unyenyekevu, Kima akamwambia, "Nimeuacha moyo wangu juu ya mwembe."

**6.** Msimulizi alifika kwa nyanya yake wakati gani?

A. Usiku
B. Asubuhi
C. Mchana
D. Jioni

**7.** Mamba aliishi wapi?

A. Juu ya mwembe
B. Mto Naisula
C. Baharini
D. Nyumbani kwa Kima

**8.** Je, unadhani ni kwa nini Mamba aliramba vidole vyake?

A. Alipenda kula maembe
B. Alitaka apewe maembe zaidi
C. Alikuwa na njaa
D. Alifurahia utamu wa embe

**9.** Funzo linalotokana na hadithi hii ni:

A. Ni jambo nzuri kuwatembelea marafiki.
B. Tunapaswa kuwasikiliza marafiki zetu.
C. Tuchague marafiki wetu kwa busara.
D. Ni rahisi kuunda urafiki.

**Swali la 10 hadi la 12**

**<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.</u>**

Jamani mtoto mwema, fahari ya watu wote
Mienendoye miema, hupendeza sisi sote
Hufanya yaliyo mema, yanayosifiwa kote
Heshima <u>silaha</u> yetu, maovu kutuepusha.

Wa kiume na wa kike, heshimu baba na nyanya
Na pia msipotoke, duniani hukanganya
Jamani wawajibike, mazuri nayo hufanya
Heshima silaha yetu, maovu kutuepusha.

Nchini mwetu angazia, haki zote kuthamini
Usawa wa kijinsia, nyumbani mpaka shuleni
Raia kujivunia, vijijini na mijini
Heshima silaha yetu, maovu kutuepusha.

**10.** Ni jambo gani ambalo mtoto mwema hafanyi?

A. Kufanya yaliyo mazuri
B. Kuwa na heshima
C. Kuwajibika
D. Kuwa na majivuno

**11.** Kwa nini heshima ni silaha?

A. Hutumiwa katika vita.
B. Humkinga mtu kutokana na maovu.
C. Hutumiwa kutekeleza maovu.
D. Humwingiza mtu hatarini.

**12.** Neno **'silaha'** limetumika katika kifungu. Kisawe cha silaha ni

A. Ngao
B. Staha
C. Amani
D. Chombo

Swali la 13 hadi la 15

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Maadili ya Mambo yalikuwa ni ya kutiliwa shaka. Mashaka alikuwa mtoto wa pekee wa wazazi wake na walimpenda kwa dhati. Hata hivyo, walimdekeza kupita kiasi. Hali hiyo ilimfanya kuwa na maringo mengi. Ujeuri ukamvaa kama nguo. Kila mara aliwatisha wazazi wake ili wampe kima fulani cha pesa kwa matumizi ya raha zake.

Waliosema kuwa mtoto umleavyo ndivyo akuavyo waligonga ndipo. Kila aliyejaribu kumkosoa Mambo alionekana kuwa adui. Alianza uvutaji sigara na kupiga mtindi. Alijipata amezama ndani ya starehe. Kiini cha haya yote kilikuwa ni kiasi kikubwa cha pesa alichopewa. Shuleni masomo yalimpiga chenga. Kila mara alikuwa chini ya matarajio kwa kila tathmini iliyofanywa. Wazazi walipogutuka, walianza kumnyima pesa, lakini wapi! Maji yakimwagika hayazoleki. Uraibu ulikuwa umemtawala.

Alianza kuiba na hatimaye akakamatwa na kukabidhiwa serikali. Alifikishwa mahakamani ambapo alikiri mashtaka. Jaji alimfunga miaka miwili gerezani.

13. Kwa nini Mambo alidekezwa?

A. Alikuwa mvulana wa pekee nyumbani kwao.

B. Alikuwa kifunguamimba

C. Alikuwa mtoto wa pekee.

D. Alikuwa na maringo.

14. Mambo alipotoka kimaadili na kuingilia anasa kwa kuwa

A. alivuta sigara na kupiga mtindi.

B. alikuwa na pesa nyingi za kutumia.

C. wazazi wake walikuwa matajiri.

D. hakufanya vizuri masomoni.

15. Maana ya neno 'alikiri' kama lilivyotumiwa katika kifungu ni

A. alikubali

B. alikataa

C. alisomewa

D. alihukumiwa

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Katika mfumo mpya __16__ kujenga nchi yetu, ugatuzi __17__ chanzo cha maendeleo __18__. Kaunti nyingi __19__ na mipango ya kuelimisha jamii kukabiliana na umaskini. Kunao viongozi ambao wamejitolea kutekeleza jukumu hili. Wanapaswa kuheshimiwa kwa kazi nzuri wanayofanya. Hakika, __20__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | A. la | B. za | C. wa | D. kwa |
| **17.** | A. umekuwa | B. imekuwa | C. yamekuwa | D. zinakuwa |
| **18.** | A. zote | B. yote | C. sote | D. lote |
| **19.** | A. itakuwa | B. litakuwa | C. imekuwa | D. zimekuwa |

**20.** A. achanikaye kwenye mpini hafi njaa

B. chanda chema huvikwa pete

C. ukubwa ni jaa

D. penye miti hakuna wajenzi

**Kutoka swali la 21 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.**

**21.** Nyati ni kwa mbogo kama vile mamba ni kwa ____________________

A. ngwena B. ngiri

C. twiga D. swara

**22.** Chagua sentensi iliyo katika kauli ya kutendea.

A. Kanini anarukaruka uwanjani. B. Wachezaji wanacheza uwanjani.

C. Yaya anamlisha mtoto. D. Mjukuu alimbebea babu yake kofia.

**23.** Chagua ukubwa wa: Mji mkubwa una watu wengi.

A. Majiji makubwa yana majitu mengi. B. Jiji kubwa lina watu wengi.

C. Jiji kubwa lina majitu mengi. D. Jiji kubwa lina majitu wengi.

**24.** **Tumia nomino ya makundi sahihi kujaza nafasi.**

Shangazi alimnunulia mtoto wake ____________________ ya viatu vipya.

A. mtungo B. jozi

C. thurea D. pakacha

25. Chagua nomino isiyopatikana katika ngeli ya U-ZI.

A. nywele

B. beti

C. nyaya

D. nguo

26. Ni sentensi gani iliyo katika hali timilifu?

A. Kitanda hakijatandikwa.

B. Matunda hujaa sokoni msimu huu.

C. Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake.

D. Paa la nyumba halikuezekwa.

27. Sentensi: "Mjomba alinunua nyanya kutoka sokoni na kuiweka kabatini" Katika wingi ni.

A. Wajomba walinunua nyanya sokoni na kuziweka makabatini.

B. Mjomba alinunua nyanya kutoka sokoni na kuziweka makabatini.

C. Wajomba walinunua nyanya kutoka masokoni na kuziweka makabatini.

D. Wajomba walinunua manyanya kutoka masokoni na kuyaweka kabatini.

28. Rafiki yako amefiwa na jamaa yake na mmekutana njiani. Je, utatumia maamkuzi gani kumjulia hali?

A. Shikamoo

B. Makiwa

C. Pole ndugu

D. Salaam aleikum

29. ***Kamilisha tashbihi:***

Roza ni kigeugeu kama ______________

A. lumbwi

B. mpingo

C. gogo

D. askari vitani

30. Jirani yako amekuwa akipatiwa msaada mara kwa mara. Amekuwa akitegemea msaada huo kwa kila jambo. Utamshauri kwa kumwambia methali gani?

A. Mui hua mwema.

B. Ndugu ni kufaana si kufanana.

C. Mtumai cha ndugu hufa maskini.

D. Haba na haba hujaza kibaba.

# TARGETER WINGS
# KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## GREDI YA 6 - MWAKA WA 2025
## SEHEMU B:
## KISWAHILI INSHA

Wings 001

*MUDA: Dakika 40*

| | |
|---|---|
| **JINA LAKO** | |
| **JINA LA SHULE YAKO** | |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*

***Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.***

***Andika insha kuhusu maelezo haya:***

***Mwandikie rafiki yako barua ukimweleza jinsi utakavyowekeza shilingi elfu moja ulizotuzwa na mwalimu wako.***